Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

*HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA*

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# CHAPISHO NA. 5

## KUWIANISHA WANYAMAPORI NA MASLAHI YA JAMII:

## UMUHIMU WA KUSHIRIKISHA SEKTA MBALIMBALI

**MASUALA MUHIMU:**

⇨ Ili kuweza kukuza mchango chanya wa wanyamapori kwa maslahi ya jamii na shughuli za kiuchumi, ni muhimu kuchukua mtazamo wa kushirikisha sekta tofauti ili kuratibu usimamizi wa wanyamapori pamoja na sekta za ardhi, utalii, misitu na mifugo.

⇨ Matendo ya usimamizi wa wanyamapori huweza kuleta migogoro na vijiji vyenye hati za ardhi hasa kupitia mwingiliano wa Mapori Tengefu na Ardhi za Vijiji.

⇨ Usimamizi wa wanyamapori na hifadhi ya misitu ya jamii katika ngazi ya kijiji vinahitaji kuwianishwa ili kutoa manufaa ya kutosha vijijini, kwa sababu wanyamapori na misitu ni raslimali zinazoweza kupatikana kwa pamoja katika ardhi za pamoja za vijiji.

⇨ Matendo na sera ya usimamizi wa wanyamapori vinatakiwa kuwianishwa na malengo ya ukuaji wa sekta ya utalii kitaifa, ili kuwanufaisha wananchi.

⇨ Usimamizi wa wanyamapori ni budi uwe na uwiano wa sera ya sekta ya mifugo pamoja na malengo ya maendeleo kwa vile wanyamapori na mifugo vyote vinategemea nyanda za malisho na vyanzo vya maji katika maeneo mengi na husababisha ushindani na wakulima.

⇨ Mtazamo wa kuhusisha sera nyingi ni muhimu ili kuweka thamani kubwa kwa wanajamii waweze kufaidika kutokana na ardhi na raslimali zilizopo.

*Kwa kushirikiana na*

policy forum · WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY · WWF · PINGO's FORUM

*© JMT 2008*

Usimamizi ulioboreshwa wa wanyamapori ungeweza kutoa manufaa mengi kwa jamii (angalia Chapisho Na. 4). Lakini pia ingeweza kusimamiwa kusaidia mahitaji ya jamii katika njia ambayo ni pana zaidi. Hii ina maana kuwa usimamizi wa wanyamapori ni budi ufikiriwe kulingana na sekta zilizopo kama vile ardhi, misitu, utalii na mifugo, kwa vile raslimali hizi zote mara nyingi hupatikana pamoja katika ngazi ya kijiji.

## Ardhi

Kupata hati za ardhi ni moja ya misingi ya maendeleo ya kiuchumi. Moja ya malengo ya Sera ya Ardhi ya mwaka 1997 ni kuhakikisha haki za kimila za kumiliki ardhi zinatambuliwa na kutolewa kisheria.

Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 zinatoa msingi wa kisheria wa kupata hati za ardhi kwa vijiji kulingana na malengo ya sera ya Taifa. Sheria hizo huunda makundi matatu ya ardhi:

- ➪ Ardhi ya Kijiji
- ➪ Ardhi iliyohifadhiwa
- ➪ Ardhi ya Jumla.

Ardhi ya Kijiji inajumuisha ardhi yote iliyotumika kimila na jamii ndani ya mipaka ya kijiji kilichosajiliwa. Ardhi iliyohifadhiwa inajumuisha maeneo yote yaliyotengwa kwa misingi ya sheria mbalimbali za kisekta, ikiwemo Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974. Ardhi ya Jumla inajumuisha ardhi nyingine yote isiyo Ardhi ya Kijiji au ardhi iliyohifadhiwa - mathalani ardhi ndani ya hatimiliki.

Kama ilivyoelezwa katika Chapisho Na. 2, Mapori Tengefu (GCA) ni ardhi iliyohifadhiwa ambako matumizi yanatawaliwa na sheria - kilimo, mifugo na makazi vinaruhusiwa. Ni karibu maeneo yote Mapori Tengefu yalianzishwa katika maeneo ambayo yamekaliwa na watu.

*Mfano*:

- ➪ Zaidi ya asilimia 90 ya ardhi Wilaya za Monduli, Simanjiro, na Longido zinaangukia ndani ya mipaka ya Mapori Tengefu. Lakini pia, maeneo haya yote yamewekwa mipaka kama ardhi za vijiji ambako wanajamii wana haki za kuishi kimila. Kwa hivyo hii hufanya maeneo haya kuwa ni 'Ardhi za Vijiji' na 'Ardhi zilizohifadhiwa' kulingana na tafsiri za Sheria ya Ardhi.
- ➪ Mgawanyo huu unaoingiliana husababisha migogoro juu ya nani mwenye mamlaka ya kusimamia ardhi hizo na anayeweza kupata hati za kumiliki kwa ardhi ambayo wananchi wanaishi katika Mapori Tengefu.



*Wanajamii wakishirikiana raslimali na wanyamapori katika Mapori Tengefu*

## Misitu

Jamii nyingi zenye wanyamapori pia huwa na raslimali misitu katika ardhi zao. Ili kukuza uwezo wa kijamii kufaidika na maliasili, ni muhimu kwa jamii kuwa na uwezo wa kusimamia kwa uwiano misitu na wanyamapori kwa pamoja.

Mara nyingi maeneo ya WMA na maeneo ya Misitu ya Hifadhi za Vijiji (VLFR) yamehamasishwa na kuanzishwa mahali pengi bila mwingiliano. Mahali pengine, misitu ya vijiji na maeneo ya WMA vimeanzishwa kwa kushabihiana.

Hata hivyo, ili jamii iweze kupata mafao zaidi kutokana na raslimali, ingefaa waweze kutumia raslimali wanyamapori na misitu (mbao, asali, madawa, kuni na majengo) katika sehemu moja. Kwa maneno mengine ina maana ni kuanzisha maeneo ya WMA na misitu ya vijiji kwa pamoja. Changamoto katika hilo linakuja katika michakato tofauti ambayo inatakiwa katika kuanzisha WMA na misitu ya vijiji.

Wakati njia za uanzishwaji wa maeneo ya WMA ni changamano na aghali, njia za uanzishwaji maeneo ya misitu ya vijiji ni rahisi. Pia, maeneo ya WMA yanasimamiwa na asasi za kijamii ambazo zinawakilisha vijiji vingi, wakati maeneo ya misitu ya vijiji yanasimamiwa na serikali za vijiji au na umoja wa serikali mbalimbali za vijiji.

Hata hivyo, njia za kuanzisha maeneo ya WMA na misitu ya vijiji katika sehemu moja zingesaidia kuhakikishia wananchi wanakuza faida kutokana na raslimali kwa kuongeza njia tofauti za mapato wanayokusanya, kama vile uvunaji, na upiga picha wa wanyamapori, mbao na mazao misitu mengine yasiyo miti.

***Kile ambacho kingeleta maana zaidi kwa jamii ni kuwa na 'maeneo ya usimamizi maliasili kijamii' ambako vyote raslimali, wanyamapori na misitu vinasimamiwa katika ngazi ya kijiji badala ya kutenganishwa kama maeneo ya WMA na misitu ya vijiji. Kupitia mazingira wezeshi ya kisera hii ingekuwa rahisi katika maeneo mengi ambayo yana vyote, WMA na misitu ya vijiji.***



*Nyika kubwa na misitu haijalindwa chini ya 'Hifadhi za Misitu' lakini badala yake zimeanza kusimamiwa na jamii*

## Utalii

Tanzania imejiwekea malengo ya kiujumla ya kuongeza wageni na mapato ya kitaifa kutokana na utalii, vilevile kuhakikisha utalii unachangia katika kupunguza umaskini ngazi ya jamii. Ili kuongeza idadi ya watalii na maduhuli, ni muhimu kwa Tanzania kuanzisha maeneo mapya ya utalii na vivutio. Tanzania ikijaribu kuongeza kiwango cha biashara ya utalii bila kupanua maeneo yanayotumiwa kwa utalii itasababisha msongamano wa maeneo nyeti na uharibifu wa maeneo hayo utafuata. Hivyo sera ya utalii Tanzania inahimiza kuendeleza maeneo mapya ya utalii na mazao ya kiutali, ikiwemo kuhimiza utalii wa kijamii.

Kwa kufikiria uwiano kati ya utalii na uwindaji ulioelezewa katika Chapisho Na. 3 kwa mtazamo wa kiuchumi, ni muhimu kufikiria malengo ya sera ya utalii ambayo Tanzania imejiwekea kwa kukuza kiwango cha biashara ya utalii. Pale utalii unapozuiwa na migogoro ya uwindaji unaweza ukakwamisha kufikiwa kwa baadhi ya malengo ya kimaendeleo. Kufikia malengo hayo kutawezekana kwa kupanua mazao ya kiutalii na maeneo katika sehemu tofauti za nchi.

## Mifugo

Tanzania ni ya tatu kwa idadi ya mifugo katika Afrika ikiwa na matazamo wa kukuza biashara ya mifugo kupitia mazao ya nyama, maziwa na ngozi. Karibu mifugo yote hiyo inamilikiwa na wakulima wadogo wadogo, ikiwa na idadi kubwa ni ya mifugo inayomilikiwa na wafugaji-wakulima. Ardhi za wafugaji-wakulima pia hushikilia idadi kubwa ya wanyamapori na vivutio vya utalii.



*Mifugo na wanyamapori vinaweza kukaa pamoja vikisimamiwa vizuri. Jamii wanahitaji sera zenye uwiano mzuri ili kutimiza hili.*

Azma ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ni "Kuhakikisha raslimali mifugo inaendelezwa na kusimamiwa ili kukuza uchumi na kuboresha maslahi ya jamii."

MKUKUTA inasema sekta ya mifugo iongeze mchango wake katika pato la Taifa, kutoka asilimia 2.7 ya 2000/01 hadi asilimia 9 kwa mwaka 2010. Hata hivyo, kupanua sekta ya mifugo kutahitaji kufanyike kwa njia ambayo inakubaliana na malengo ya sekta zingine, kama vile wanyamapori na utalii ili kuhahikisha ukuaji wa sekta moja hauhafifishi ukuaji wa sekta nyingine.

Njia moja ya kufanya hili ni kuwapatia hatimiliki jamii za kifugaji ili kusimamia manufaa kutokana na wanyamapori na kujibu matatizo yanayokabili maeneo ya WMA kama ilivyoelezwa katika Chapisho Na. 4. Jambo muhimu ni kusaidia uzalishwaji wa mifugo kupitia desturi za matumizi ya ardhi ya kifugaji na kutambua kuwa uanzishwaji wa ufugaji wa kibiashara katika ranchi zilizowekewa uzio kutasababisha kupungua kwa idadi ya wanyamapori na hivyo kupunguza uwezo wa kiutalii.

***Njia nzuri ya kufikia ukuaji endelevu kwa sekta ya mifugo katika nyanda za malisho ni kuhakikisha kuwa mifumo ya matumizi ya ardhi inaweka uwiano baina ya wanyamapori, utalii na uzalishaji wa mifugo.***

Kuwianisha maboresho katika usimamizi wa wanyamapori, maendeleo ya utalii, uzalishaji wa mifugo unawezekana, lakini itahitaji ujanja wa mtazamo wa kisekta. Uwiano huu ni muhimu si tu kuwafaidisha wananchi kutokana na raslimali zao, lakini pia kuhakikisha matumizi ya ardhi yanayowianisha wanyamapori na mifugo kushindana na shughuli mbadala kama vile kilimo ambacho hutowesha vyote, mifugo na wanyamapori.